

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Kwanza – Tarehe 5 Septemba, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, karibuni sana kwenye Mkutano wetu wa Nane ambao unaanza leo tarehe 5 Septemba, 2017 na leo ni kikao cha kwanza. Tunamshukuru Mungu kwamba tulikwenda Majimboni, tumeshughulika na shughuli za wananchi na sasa tumerudi tena kwa shughuli nytingine za wananchi na kwa faida ya nchi yetu.

Sasa tunaendelea na shughuli. Katibu.

DKT. THOMAS KASHILLILAH – KATIBU WA BUNGE:

KIAPO CHA UAMINIFU

Wabunge wafuatao waliapa:-

- (i) Mhe. Alfredina Apolinary Kahigi
- (ii) Mhe. Kiza Hussein Mayeye
- (iii) Mhe. Nuru Awadh Bafadhili

- (iv) Mhe. Rukia Ahmed Kassim
- (v) Mhe. Shamsia Aziz Mtamba
- (vi) Mhe. Sonia Jumaa Magogo
- (vii) Mhe. Zainab Mndolwa Amir

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwanza nawapongeza sana waliokuwa Wabunge Wateule, sasa mmekamilisha utaratibu na mchakato. Kwa niaba ya Wabunge wenzeno wote kabisa na wananchi kwa ujumla, tunasema hongereni sana na karibuni sana Bungeni. Tutawapa kila aina ya ushirikiano na ninawaomba Ofisi ya Katibu iwapatie zile fomu za kuchagua Kamati haraka sana ili muweze kupangiwa Kamati na muanze kazi leo leo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kiapo hiki cha uaminifu walichoapa wenzetu leo asubuhi, kinatukumbusha wengine wote ambao tuliapa muda mrefu kidogo utii wetu kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kiapo chetu kwa ujumla wake kuhusiana na uaminifu na utii kwa Katiba na nchi yetu.

Kwa hiyo, tukumbushe wengine wote kwamba hicho ndiyo kiapo chetu. Ni vizuri kuisoma Katiba na kuipitia. Ndani mle kuna nafasi ya Vyama vya Siasa na uhusiano wa Mbunge na Chama cha Siasa. Huwezi ukawa Mbunge bila kuwa Mwanachama wa Chama cha Siasa na ziko taratibu zake. Kwa hiyo, taratibu zote zilifuatwa kwa Waheshimiwa hawa kuingia hapa Bungeni na zimekamilika. Karibuni sana.

Kwa kumalizia tu, pia Spika ana nafasi yake jamani, mimi si huwa nasema hapa! Huwa nasema hapa. Wako baadhi ya lile kundi, wiki mbili kabla ya mambo haya kutokea, kukawa na magazeti kama mawili matato yamejaa ukurasa wa katikati pale, baadhi ya wale wanajinasibu, wanasema; "Spika huyu ni dhaifu." Yale maneno yao yale, "Spika dhaifu," ilipofika kwenye 18 nikasema sasa udhaifu wangu hapa ndiyo utakaoonekana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama una akili yako, maneno hayana umuhimu, kwa sababu huyo unayesema dhaifu, *after all* sio dhaifu. Sasa mwisho wake utaumia bure tu.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuendelee. Katibu.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

**Mchango wa Serikali Kukamilisha Vituo
Vipya Vya Afya na Zahanati Ikungi**

MHE. ELIBARIKI E. KINGU aliluliza:-

Wilaya ya Ikungi hasa Jimbo la Singida Magharibi inakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa vituo vya afya na zahanati. Aidha, umbali mrefu wa kutafuta matibabu umekuwa ukisababisha adha na taabu kwa wananchi wa kata za Lyandu, Igelansomi na vijiji vya Mduguya, Kaangeni, Chengu na Mayahu.

Je, Serikali ipo tayari kushirikiana na wananchi katika kukamilisha ujenzi wa zahanati mpya na vituo vya afya viliyvoanzishwa kwa ushirikiano wa wananchi na Mbunge?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza miradi ya vituo vya kutolea huduma za afya kwa kushirikisha nguvu za wananchi kuititia mpango wa fursa na vikwazo yaani *O & OD*. Serikali inampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la

Singida Magharibi na wananchi wake kwa kuanza ujenzi wa vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Spika, katika kuunga mkono juhudhi hizo, Serikali imetoea ruzuku ya maendeleo kwa Halmashauri hiyo, kiasi cha shilingi milioni 110 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya na zahanati katika Wilaya ya Ikungi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.49 kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa maboma yaliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Kingu, nimekuona, swalii la nyongeza.

MHE. ELIBARIKI E. KINGU: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya kaka yangu Mheshimiwa Jafo, nilikuwa nataka nipate hakikisho kwa sababu hivi tunavyozungumza mimi na wananchi tumeanzisha ujenzi wa zahanati katika vijiji 19 kwa nguvu zetu.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atanihakikishia kwamba zahanati hizi za Nkunikana, Puma, Msambu, Unyangwe, Chungu, Kinyampembee, Mpetu, Mayaha, Misake, Maswea, Nsogandogo, Kipunda, German, Mahonda, Iyumbu, Mlandala, Kaugeri, Mduguyu, Mpugizi na Namnang'ana ambazo tumezianzisha kuzijenga ndani ya kipindi cha miaka miwili katika huu mgao, Mheshimiwa Naibu Waziri ananihakikishia kwamba na zenyewe zinakwenda kukamilishwa? Hizi ambazo tumezianzisha sisi.

SPIKA: Mheshimiwa Elibariki, Puma hakuna zahanati mpaka leo? Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyo sema pale awali, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Kingu kwa kazi kubwa anayofanya katika ile Wilaya yote ya Ikungi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa bajeti wa mwaka huu tumetenga karibuni shilingi bilioni 251 katika *Local Government Development Grants*, lakini katika hizo karibu shilingi bilioni 68 kwa ajili ya kuboresha vituo vya afya na zahanati, yaani yale maboma yaliyojengwa. Katika hizo nilisema pale awali *1.4 billion* ni kwa ajili ya Halmashauri ya Ikungi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu Kamati ya Fedha itakapokaa pale, katika vipaumbele vya umalizaji wa maboma, haya maeneo ambayo tumesema tutawaletea fedha, basi ni vyema katika ule mpango ni lazima tuhakikisha maboma haya yamekamilika kwa sababu Serikali ndiyo imeshafanya jambo lake hilo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Mheshimiwa Kingu alileta *concern* kubwa ya Halmashauri yake kuhusu changamoto ya afya. Ndiyo maana kama Serikali kwa ujumla, hivi sasa tunawapelekea fedha za kwanza, karibu shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya pale lhanja ambapo tunajua pale kutakuwa na *theater* kubwa na maabara. Kwa hiyo, eneo lile litabadilika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutakuwa na fedha nydingine kwa ajili ya ununuzi wa vifaa. Kwa hiyo, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba wananchi wa Halmashauri yote ya Ikungi inapata huduma nzuri kama tunavyotarajia.

SPIKA: Mheshimiwa Massare nilikuona, swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Matatizo yaliyoko huko Singida Magharibi yanafanana kabisa na yaliyoko katika Jimbo la Manyoni Magharibi, na sisi tumeanza kujenga zahanati nyngi.

Je, Serikali iko tayari sasa kuiongezea mgao Halmashauri ya Itigi ili iweze kufunika maboma ambayo tayari tumeしゃanza katika vijiji vya Mbugani, Mnazi Mmoja, Tulieni na vijiji vingine vingi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ni kweli anachoshuhudia Mheshimiwa Mbunge kwamba tulipofika pale Itigi katika Halmashauri ya Itigi, lakini bahati mbaya wao hawana Hospitali ya Wilaya. Ndiyo maana mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba Halmashauri ile ambayo kwa jiografia yake mara nyingi wanatumia kile Kituo cha Kanisa kama ndiyo sehemu kubwa ya utoaji huduma ya afya, Serikali hatutasita kutoa ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, katika ule mpango ambaeo fedha ambazo tumetenga; na Halmashauri hii tutaipa kipaumbele. Kwa hiyo, Mkurugenzi ahakikishe yale maboma yaliyoanzwa kujengwa, yamemilika. Hata hivyo, kuna mpango kwamba, tutaisaidia Itigi *as a special case* kuona ni jinsi gani wananchi wa Manyoni Magharibi wataweza kupata huduma nzuri.

SPIKA: Ahsante sana. Swali linalofuata, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, tafadhalii.

Na. 2

**Shule ya Sekondari ya Mpanda
Kuishia Kidato cha Nne**

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE aliuliza:-

Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda ilikuwa ya bweni kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne, lakini sasa imekuwa ya kidato cha tano na sita tu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuirejesha shule hiyo kama ilivyokuwa awali?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda ilisajiliwa kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita pekee ili kukidhi malengo ya kuwa na shule za kutosha za Kitaifa katika Mkoa wa Katavi. Shule hii ni mionganini mwa shule saba za sekondari zenye kidato cha tano na sita katii ya shule 38 za sekondari zilizopo Mkoani Katavi. Kutokana na mwitikio mkubwa wa wananchi kwa kushirikiana na Serikali katika ujenzi wa shule za sekondari za kutwa za kidato cha kwanza hadi cha nne, Serikali imeona umuhimu wa kuongeza shule ya kidato cha tano na sita ikiwemo Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mpanda.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kila Tarafa inakuwa na sekondari ya kidato cha tano na sita. Serikali inatambua nia njema ya Mheshimiwa Mbunge kwa watoto wa eneo hilo. Hata hivyo, kama kuna ulazima wa kufanya hivyo, inahitajika maombi yafanyike kupitia taratibu husika za usajili wa shule. Serikali inaendelea kuboresha shule za kata zilizoko Mkoani Katavi ili kupunguza msongamano na kutoa elimu bora.

SPIKA: Mheshimiwa Kikwembe, nilikuona, swalii la nyongeza.

MHE. DKT. PUDENSIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumweleza kwamba, pamoja na kwamba Serikali ina nia njema ya kuweka sekondari za wasichana kila tarafa na kwa sasa katika Jimbo langu ama Mkoa wa Katavi kila tarafa bado haijawa bado na Sekondari za *form five* na *six*.

Je, haoni sasa kuna umuhimu na ulazima wa hii Shule ya Sekondari ya Mpanda kuanza sasa kwa kidato cha kwanza mpaka cha sita ili tuweze kuzula mimba za utotoni kama sera na Serikali inavyosema?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kama Serikali, tunaona umuhimu hasa wa kupunguza mimba za utotoni na kwa wasichana ambao Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiwapigania hapa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kama ikiwezekana basi mchakato huo utaanza katika vikao husika kuanzia Baraza la Madiwani *then* itaenda katika Kamati ya Ushauri ya Mkoa, *then* itafika kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya sekta ya elimu na hapo akiridhia jambo hilo basi litaanza. Kwa hiyo, hili jambo halina mashaka, ni suala zima la kuangalia ni jinsi gani tutafanya.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tunasisitiza na Serikali inaweka nguvu ya kutosha na kama kuna changamoto kubwa, tutaona jinsi gani tutafanya ikiwa hata kuanzisha shule nyingine mpya zenye ubora unaofanana na ule. Lengo kubwa ni kuhakikisha watoto wetu hasa wasichana wawewe kusoma katika mazingira rafiki tupate viongozi na wataalamu wa baadaye.

SPIKA: Mheshimiwa Hawa Ghasia, nilikuona, swali la nyongeza.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi napenda kuuliza swali la nyongeza.

Swali ambalo Mheshimiwa Kikwembe ameuliza ni kwamba katika shule nyingi ikiwemo Ndanda Sekondari, Loleza na shule nyingi ambazo zililbadilishwa, zilizokuwa za wasichana na wavulana zikawa za wavulana. Hata hivyo,

hizo shule hazijai kwa sababu shule ambayo ilikuwa kidato cha kwanza mpaka cha sita, leo unaifanya ya kidato cha tano tu na cha sita. Mabweni ni mengi. Nenda Loleza, hayajai; Ndanda hayajai; *Mtwara Girls* na shule nyingine nyingi. Maombi tayari yalishakuwa yamefika TAMISEMI na mchakato wa kufanya tathmini ulishaanza.

Je, ule mchakato ulisimama kwa tatizo gani? Nilichokuwa namuomba Mheshimiwa bado warudi wakalifanyie tathmini suala hilo kwa sababu majengo mengi yako *idle* na wanafunzi hasa wa kike wanakosa pa kwenda?

SPIKA: Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tamisemi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa *concern* ambayo na sisi Serikalini tunajaribu kuitafakari. Maamuzi haya yalipofanyika pengine hatukufanya uchambuzi vizuri. Kuna faida kubwa shule inapokuwa na *O-level* na *A-level* kwa pamoja kuliko unapoamua *A-level* wakawa peke yake na *O-level*/wakawa peke yake.

Hata hivyo, tunaendelea kuwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Elimu ili tuweze kuona namna ya kurudisha kwa haraka tu, kwa sababu ni suala dogo tu; kurudisha ile miundombinu ipo na pengine maeneo mengine miundombinu imekuwa ikiharibiwa kwa sababu haitumiki. Kwa hiyo, *concern* ya Mheshimiwa Hawa Ghasia ni ya kweli na tutajaribu kuchambua kwa shule zote nchi nzima tuweze kuona namna ya kuzirudisha shule katika mfumo ule wa zamani ulivyokuwa. (*Makofii*)

SPIKA: Bahati nzuri na Profesa Ndalichako yuko hapa, naamini wazo hili kwa kweli ni zuri la kufanyiwa kazi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la tatu kwa siku ya leo, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Susanne Peter Masele, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 3

Kusitishwa kwa Mikataba ya Ajira Nchini

MHE. SUSANNE P. MASELE aliuliza:-

Tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani, imekuja na mikakati yake mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhakiki watumishi wa umma, zoezi ambalo halikuwekewa muda wa kuanza na kumaliza (*time frame*) hali hiyo imesababisha usumbufu mkubwa na hata kuharibu mfumo wa watumishi wa umma, ikiwemo namna ya kuajiri.

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa watumishi wa umma walioajiriwa na kusainishwa mikataba ya ajira ndani ya Serikali ambapo ghafla mwaka 2016 Rais alitoa kauli ya kusimamisha ajira kupisha ukaguzi wa watumishi hewa?

(b) Je, Serikali inatambua kuwa watu hao tayari walikuwa watumishi na mchakato wa kuwaingiza kwenye *payroll* ulishaanza, lakin ukasitishwa ghafla na sasa wako mtaani na hawajui hatma yao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susanne Peter Masele, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba watumishi wote ambao walisitishwa kuingizwa katika orodha ya malipo ya mishahara (*payroll*) mwezi Mei, 2016 waliokuwa wakipisha zoezi la uhakiki wa watumishi wamesharudishwa katika orodha ya malipo na sasa wanaendelea na kazi na wamekuwa wakilipwa mishahara yao kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) ya swali la Mheshimiwa Masele, watumishi hao wanatambuliwa kama watumishi wengine wa umma.

SPIKA: Mheshimiwa Susanne nimekuona.

MHE. SUSANNE P. MASELE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Ni lini sasa Serikali itaondoa hii dhana ambayo imeanza kujengeka kwamba Serikali haiwezi kuajiri kwa sababu haina fedha na kwamba Mheshimiwa Rais ndiye amekuwa akiajiri kwa utashi wake bila kufuata sheria?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali inajigamba kwamba imekusanya mapato mengi na imeondoa Wafanyakazi hewa, lakini ni kwa nini haijapandisha mshahara wala kupandisha watu madaraja? Serikali iwaambie Watumishi, ni kwanini haifanyi hivyo? (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawal Bora, Mheshimiwa Angella Kairuki. Kwa nini hamfanyi hivyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa napenda kusema hakuna dhana kwamba Serikali haina uwezo wa kuajri. Wote mnafahamu katika mwaka wa 2015/2016 mazoezi yaliyokuwa yakiendelea katika uhakiki, lengo letu kubwa lilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na idadi ya rasilimali watu ambayo tuna uhakika nayo, pia kujiriddhisha fedha ambayo tunalipa kama kweli ni thamani ya fedha kulingana na rasilimali ambayo ipo kazini.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa kufanya hivyo, tumeweza kuondoa zaidi ya watumishi hewa 19,708 ambao endapo wangeendelea kubaki katika orodha ya malipo ya mshahara, wangeisababishia Serikali hasara kila mwezi ya

zaidi ya shilingi bilioni 19.8 fedha ambazo zingeweza kwenda kutumika katika miradi mingine ya maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tu katika mwaka huu wa fedha, tayari katika bajeti yetu tuliji-*commit* kama Serikali kwamba tutatoa ajira katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 zaidi ya ajira 52,436. Pia tumeshaanza, ukiangalia katika mwaka huu wa fedha ambao tulikuwa tunaumalizia mpaka Julai, tayari tumeshatoa zaidi ya vibali vya ajira 10,184 na zaidi ya vibali vingine 4,816 pia viko katika taratibu za kutolewa kwa ajili ya kuziba mapengo yaliyojitekeza kutohana na suala zima la vyeti vya kughushi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala zima la kupandisha mishahara pamoja na vyeo au madaraja; katika suala la mishahara, mwaka huu kilichofanyika na nimekuwa nikilisema mara nyingi, ni kweli hatujapandisha mishahara. Hatujapandisha mishahara kwa sababu bado tunaendelea kuangalia hali ilivyo, pia na hali ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, tulichokifanya kwa mwaka huu ni nyongeza ya miashahara ya mwaka ambayo ni *annual increment* na wakati wowote kuanzia sasa nyongeza hiyo ya mishahara ya mwaka itaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madaraja, tayari fedha ilishatengwa. Kuna zaidi ya shilingi bilioni 660 zimeongezeka katika bajeti ya mwaka huu ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2016 iliyoleta shilingi trilioni 6.6. Mwaka huu tumetenga zaidi ya shilingi trilioni 7.205 na hii itasaidia kulipa maadeni ya watumishi, itasaidia pia kupandisha watumishi zaidi ya 193,166 na tunaamini wakati wowote stahiki hizo watumishi wataweza kuzipata.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo maelezo ya Serikali na hakuna dhana ilijoengenka kwamba hatuwezi kuajiri wala kupandisha mishahara. (*Makofit*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba waliondoa watumishi hewa 19,708. Ni dhahiri kwamba kuondolewa kwa wafanyakazi wenye vyeti *fake* kumeathiri zaidi maeneo ya elimu na afya. Napenda kujua *statistically* ni vipi Serikali, maana yake ametuambia wataajiri; mpaka sasa hivi Serikali imeajiri walimu wangapi na wafanyakazi wa sekta ya afya? Maana yake kuna zahanati nyingine hazina kabisa watumishi.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine unakuta shule zina walimu watatu tu, tunaweza kuona ni madhara gani watoto wetu watapata. Sasa kama walikuwa na hili zoezi la vyeti *fake*, walijiandaa vipi *ku-replace* hawa wafanyakazi kwenye sekta ya elimu na afya? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa kama nilivyoeleza, tumeshatoa vibali hivyo 10,184 na sasa hivi kwa upande wa elimu, tayari Wizara ya Elimu imeanza zoezi la kuchambua, wanatuma vyeti wale ambao walikuwa ni wahitimu na wanaostahiki kuingia, baada ya hapo watahakikiwa na kuweza kuingia katika ajira.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika walimu kwa ujumla wake, katika *ku-replace* watumishi ambao wameondoka kwa walimu, ni zaidi ya walimu 3,012 wataweza kuajiriwa katika zoezi hili. Pia katika suala zima la sekta ya afya, tutaja zaidi ya watumishi 3,152. Hili ni katika kuziba pengola walioghushi vyeti feki. Baada ya hapo, katika mwaka wa fedha 2017/2018 ajira bado ziko pale pale 52,436 na ni kutokana na hali ya uwezo wa kibajeti.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, sijui ni hii mambo ya vyeti *fake*, Bungeni nako tuangalie angalie nini, kidogo. (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

SPIKA: Alah, mnapiga makofi eeh! Nitamwagiza Katibu sasa hivi! Kwa kuwa wengine wamenuna, basi hilo hapana, halitekelezwi. (*Kicheko/Makofi*)

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah.

Na. 4

Umuhimu wa Kufufua Reli ya Kusini

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH aliuliza:-

Katika miaka ya 1950 Lindi kulikuwa na reli inayotoka Nachingwea kupitia Mtama, Mnazi Mmoja, Mingoyo hadi Bandari ya Mtwara na ilikuwa ikisafirisha korosho, mbao, magogo na watu. Kwa sasa Lindi kuna viwanda vingi na vingine vinatarajiwa kujengwa, barabara ya Kibiti – Lindi ambayo hupitisha mizigo mizito huenda ikaharibika mapema, hivyo reli ni muhimu sana.

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuifufua reli ya Kusini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara inaunganishwa kwa reli ili kutumia Bandari kubwa ya Mtwara katika kusafirisha mizigo mbalimbali, Serikali imeshafanya upembusi yakinifu wa reli ya Mtwara hadi Mbamba Bay ambapo inatarajiwa reli hiyo ijengwe kwa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (*PPP*). Baada

ya kukamilika kwa reli ya Mtwara hadi Mbamba Bay utaratibu wa kuunganisha Lindi na Mtwara kwenye reli utafuata.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kumwajiri Mshauri wa Uwekezaji (*Transaction Advisor*) atakayekuwa na jukumu la kuunadi mradi kwa ajili ya wawekezaji mbalimbali na hatimaye kujenga reli ya Mtwara hadi Mbamba Bay na matawi ya kwenda Liganga na Mchuchuma yenye jumla ya urefu wa kilometra 1,000. (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Hamida, swali la nyongeza.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu haya yenye matumaini kwetu wananchi wa Mikoa hii ya Kusini, kwa sababu sasa tunaona Serikali inafanya jitihada kubwa sana katika kuharakisha maendeleo kwa Mikoa hii ya Kusini. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri ambayo tunaisubiri kwa hamu kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kujua, baada ya ujenzi huu wa reli hii ya Mbamba Bay kukamilika, halafu itakapokuja katika eneo hili la Mtwara – Lindi.

Je, ujenzi huu wa reli ya Mtwara - Lindi utaishia Lindi tu au itakuwa Mtwara – Lindi – Dar es Salaam? Napenda kujua hilo, ahsante sana.

SPIKA: Swali fupi la nyongeza, majibu mafupi Naibu Waziri, Mheshimiwa Edwin Ngonyani, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuendeleza Mikoa ya Kusini katika masuala ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kutupongeza na nimwahidi kwamba reli ambayo tunaiongelea hapa ni ile

ambayo ilikuwepo zamani ambapo ilikuwa inatoka Mtwara – Lindi inapita Mnazi Mmoja na ilikuwa inaishia Liwale. Hoja ya kujenga reli kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam hatujawahi kufikiria. Tumesikia na tutaendelea kulitafakari hilo suala.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata. Kwa sababu ya muda, Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum, swali lako tafadhali.

Na. 5

**TANROADS Kusimamia Barabara Zinazoelekea
Bonde la Ziwa Tanganyika**

MHE. SILAFU J. MAUFI aliuliza:-

Kata ya Kula ipo kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika umbali wa takribani kilometa 50 kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi huku kukiwa hakuna barabara ya kuunganisha kata hiyo yenye mawe mengi na miteremko mikali kufika huko.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuzichukua barabara zenyе kuelekea Bonde la Ziwa Tanganyika na kuwa chini ya *TANROADS*?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna barabara tatu zinazoelekea katika mwambao wa Ziwa Tanganyika ambazo zinaunganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi. Barabara hizo ni Nkana – Kala ambazo urefu wake ni kilometa 67, Kitosi - Wampembe yenye urefu wa kilometa 68 na Namanyere hadi Ninde yenye urefu wa kilometa 60 ambazo pia zinaunganisha

Makao Makuu ya Kata za Kala, Wampembe na Ninde. Barabara zote hizi zinasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

Mheshimiwa Spika, maombi ya kupandisha hadhi barabara mbili kati ya tatu nilizozitaja, tayari yamewasilishwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Tathmini ya Wizara baada ya kuyapitia maombi hayo ilibainisha kuwa Barabara za Nkana hadi Kala yenyе urefu wa kilometa 72 na Kitosi hadi Wampembe yenyе kilometa 68 hazikidhi vigezo vya kupandishwa hadhi kuwa barabara ya mkoa. Hivyo ilipendekezwa zibaki katika hadhi ya sasa. Kwa upande wa barabara ya Namanyere hadi Ninde yenyе kilometa 60, kumbukumbu za Wizara zinaonesha haijawahi kuombewa kupandishwa hadhi.

Mheshimiwa Spika, kutoчana na Serikali kuanzisha Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (*TARURA*), barabara zote zitaendelea kuhudumiwa na *TARURA* chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

SPIKA: Mheshimiwa Silafu, swali la nyongeza.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya kitaalam ambayo kwa namna moja au nyingine akina mama zangu wa Mkoa wa Rukwa na hususan wa Bonde la Tanganyika, bado hawajatendewa haki. Tunasema ya kwamba tunazuia magonjwa na vifo vya wamama na watoto, katika maeneo haya hatutakuwa tumezuia vifo vya akina mama na watoto, bali tutaendeleza vifo hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa Mheshimiwa Waziri anahusika vilevile na suala zima la mawasiliano, afahamu ya kwamba kata ya Kara haina mawasiliano ya barabara na wala haina mawasiliano ya simu. Huu utaalam wa *TARURA* watakuwa wamewapa umuhimu upi wa kuweza kuyafanya kazi katika hizi barabara zetu za Ziwa Tanganyika na vilevile zinazoelekea kwenye barabaa za Ziwa Rukwa ziko katika hali hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kupata majibu yaliyokuwa sahihi hasa kuhusu akina mama zangu wa Bonde la Tanganyika na Bonde la Rukwa, wanasaidiwa vipi juu ya hizi barabara na hao ndugu wa *TARURA*?

SPIKA: Majibu ya swali holo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi kwa namna anavyoshirikiana na Wabunge wenzake katika kufuatilia masuala mbalimbali ya maendeleo ya watu wa Mkoa wa Rukwa na vilevile Mkoa wa Katavi. Sina uhakika kwa nini wanashirikiana wakati ni watu wa mikoa miwili tofauti, lakini nadhani ni kwa sababu maeneo yao yanafanana. Mara nyingi barabara anazoziongelea nyingine zinaunganisha mikoa yote hii miwili, kwa mfano, barabara zinazoenda kwenye Ziwa Rukwa zinapita katika mikoa hii yote miwili.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie, kama ambavyo tumeweka katika bajeti, barabara hizo tutazishughulikia kwa kadiri bajeti ilivyopangwa. Kwa mfano, barabara inayounganisha mikoa hiyo miwili, lakini vilevile na Mkoa wa Songwe anafahamu kwamba tumeanza kujenga daraja linalounganisha mikoa hiyo na tukishamaliza kujenga daraja, tutaanza sasa kuiangalia barabara yenye.

Mheshimiwa Spika, kubwa nimhakikishie kwamba Serikali inafahamu sana na wala haina nia hiyo anayoiongelea. Barabara hizo zitashughulikiwa na *TARURA* kwa kiwango na kwa kasi ile ile ambavyo angetegemea kwa kuzipandisha hadhi. Kwa sababu *TARURA* na *TANROADS* kwa sasa wana hadhi sawa na uwezo sawa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hata kwenye upande wa rasilimali fedha nako huko tunakuangalia, ili kuhakikisha taasisi hizo mbili zinatekeleza ahadi zetu na ahadi za viongozi katika maeneo hayo ambayo yameulizwa kwa kasi na kiwango kinachotakiwa.

SPIKA: Mheshimiwa Lubeleje, nilikuona. Swali fupi la nyongeza.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza napenda niipongeze sana Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuanza kujenga barabara ya lami kuanzia Mbande kwenda Kongwa - Mpwapwa mpaka Kibakwe. Sasa swali langu ni hivi, je, hii barabara ikishafika Njia Panda ya Kongwa inaendelea moja kwa moja mpaka Mpwapwa? Hilo ndiyo swali langu. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo muhimu. Hata hapo Mbande - Kongwa kwenyewe bado ni nusu tu. Utamalizia hapo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbande – Kongwa – Mpwapwa mpaka Kibakwe ni barabara moja. Tumeianza na tutahakikisha tunaikamilisha kama ambavyo imeandikwa katika Kitabu cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 hadi 2020.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hatuishii Kongwa, tutaendelea na ujenzi wa hiyo barabara kama ambavyo kwenye Ilani tumeahidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii nisema kwamba wakati nikitembelea barabara hii, wananchi wa Kongwa walikusifu sana. Na mimi niombe nichukue fursa hii, pamoja na kwamba pengine siyo sahihi, lakini ni muhimu nizifikishe zile sifa za wananchi wa Kongwa ambaao walikuwa hawategemei kama hiyo barabara tutajenga. Na mimi niliwahakikishia hii barabara iko katika ilani na ahadi zote tulizoweka katika ilani tutazikamilisha pamoja na barabara hii ya kutoka Mbande – Kongwa – Mpwapwa hadi Kibakwe kwa Mheshimiwa Simbachawene.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi. Mheshimiwa Omari.

Na. 6

Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Kilindi - Gairo

MHE. OMARI M. KIGUA aliuliza:-

Mwaka 2014 Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne alitoa ahadi ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Kilindi hadi Wilaya ya Gairo.

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hiyo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kilindi kuanzia Songe kuelekea Gairo ina urefu wa kilometra 111.29. Sehemu ya barabara hii kutoka Songe hadi *Kwekivu Junction* na mpaka lyogwe yenye urefu wa kilometra 69.5 inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania Mkoo wa Tanga na sehemu ya barabara ya lyogwe hadi Chakwale mpaka Ngilori yenye urefu wa kilometra 41.79 inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) kwa Mkoo wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, barabara hii imekuwa ikitengewa fedha kila mwaka na kufanyiwa matengenezo ya kawaida, matengenezo ya muda maalum, matengenezo ya sehemu korofi, ujenzi wa madaraja na matengenezo makubwa ya madaraja. Matengenezo haya yameifanya barabara hii iweze kuitika majira yote ya mwaka. Aidha, mwaka 2014 Mheshimiwa Rais Mstaafu, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alitoa

ahadi ya kujengwa kwa kiwango cha lami kwa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha kuwa barabara hii ya kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Kilindi inayoanzia Mji wa Songe hadi *Kwekivu Junction* - lyogwe - Chakwale hadi Ngilori, Wilaya ya Gairo yenyе urefu wa kilometa 111.29 inaingizwa kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hii kiuchumi na kijamii, Serikali itaendelea kuifanya matengenezo ya aina mbalimbali ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Omari, swali la nyongeza.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Ujenzi, napenda kuuliza swali moja la ziada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba barabara hii ni muhimu sana kiuchumi na ukizingatia kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Kilindi kwa maana ya Songe hadi Gairo ni kilometa hizo alizotaja. Barabara hii nyakati za mvua ina changamoto kubwa sana na ni juzi tu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya alipokuwa anakuja Makao Makuu ya Wilaya, alikwama maeneo ya Chanungu pale kwa takribani saa mbili.

Swali langu linakuja, je, ni lini sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atahakikisha kwamba watu wa *TANROADS* Mkoa wa Tanga wanasmamia kwa dhati matengenezo maeneo yafuatayo, kwa maana katika Bonde la Chanungu, Kijiji cha Mafulila pamoja na eneo la Kikunde, karibu kabisa na Kijiji cha Gairo hapa kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika kwa msimu mzima wa mwaka?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineeer Ngonyani*.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilieleza katika jibu la swali la msingi, barabara hii ni muhimu sana na Serikali inalifahamu hilo.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilisema, tunatenga bajeti ya fedha na mwaka huu zimetengwa kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika majira yote. Kwa sababu hiyo, nawaelekeza *TANROADS* Mkoa wa Tanga na *TANROADS* Mkoa wa Morogoro kuhakikisha barabara hii inapitika majira yote. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda kama mnavyojua leo tulianza na shughuli maalum; Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mbunge wa Mgogoni

Na. 7

Kuwepo kwa Mahakama Kuu Mbili – Tanzania

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF aliuliza:-

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazo Mahakama Kuu mbili, ile ya Jamhuri ya Muungano na ile ya Zanzibar.

(a) Je, ni Mahakama ipi ipo juu ya nyingine?

(b) Je, kuna utaratibu gani wa ushirikiano katika kusimamia kesi au mashauri ambayo yanaanza upande mmojawapo wa Muungano?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mbunge wa Mgogoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 108 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, kwa mujibu wa Muundo wa Mahakama katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuna Mahakama ya Zanzibar iliyotamkwa katika Ibara 114 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 93 ya Katiba ya Zanzibar. Mahakama zote tajwa zina hadhi sawa katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, upo ushirikiano katika masuala ya utekelezaji wa amri za Mahakama katika suala linaloanza upande mmoja wa Muungano ambalo limeshughulikiwa na kufikia mwisho. Ingawa kama ilivyoelezwa hapo juu, kila Mahakama ina hadhi sawa na nyingine na hivyo shauri lililoanza kusikilizwa upande mmoja, haliwezi kuhamishiwa upande wa pili ili kukamilisha usikilizwaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, shauri likianza kusikilizwa, linapaswa kusikilizwa na kuhitimishwa na Mahakama Kuu ya upande husika wa Muungano.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Suleiman.

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ikiwa Serikali inayaamini haya majibu walionipa, swali la kwanza, je, haioni kwamba kuwashamisha Masheikh ambao mnawatuhumu kwa ugaidi kutoka Zanzibar kuja kushitakiwa Bara, ni kuinyang'anya Mahakama ya Zanzibar mamlaka yake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ukisoma *Tanzania Law Reports* ya mwaka 1998, ukurasa wa 48 inayohusu kesi ya Maalim Seif Shariff Hamad akipingana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inasema wazi kwamba iwapo mtu atafanya kosa Zanzibar kwanza anapaswa kushtakiwa Zanzibar, pili anapaswa kushtakiwa na Mahakama ya Zanzibar. Swali linakuja hapa ni sheria ipi iliyotumika kuwahamisha Mashekhe kutoka Zanzibar ambao ni Wazanzibar kuja kushtakiwa katika Mahakama za Bara? (*Makofi*)

SPIKA: Mbona mnafanya fujo, inakuwaje tena?
(*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, sipingani na muuliza swali kwenye upande wa vipengele vya kisheria lakini naomba tu nimwambie kwamba kuna makosa ambayo *specifically* siyo ya kijiografia. Kwa mfano, kama watu watafanya makosa ya kung'oa michikichi Kigoma hilo unaweza ukalitaja kama ni kosa la Kigoma. Kama watu watang'oa mikarafuu Pemba unaweza ukasema kwamba hilo ni kosa liliofanyika Pemba na ni karafuu ya Pemba, lakini yanapofanyika makosa ambayo ni ya nchi nzima, Mtanzania ama raia ye yeyote awe wa Tanzania ama nje ya Tanzania atachukuliwa na taratibu za kufuata haki/sheria zitafanyika pale ambapo mamlaka inayochukua hatua hizo inaona ndipo panapofaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya ambayo muuliza swali ameuliza yanaendelea kubakia kwa maeneo na makosa ambayo yamefanyika na ni mahsus i katika eneo husika na hicho ndicho kinachofanyika. Hatua zote zitaendelea kujulikana kadiri hatua zinavyochukuliwa na upelelezi unavyofanyika. (*Makofi*)

SPIKA: Nyongeza ya majibu, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu kama yapo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Hamna.

SPIKA: Imetosha eeh?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Ndiyo.

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuona Mbunge mpya Mheshimiwa Rukia Ahmed Kassim, karibu tena Bungeni. (*Makofii*)

MHE. RUKIA AHMED KASSIM: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Zanzibar Sheria ya Makosa ya Kimtandao (*CyberCrime Act*) bado haijapitishwa, je, inapotokea Mzanzibar kamtendea kosa Mzanzibar mwenzie yaani makosa ya mtandao, naweza kumfungulia kesi katika Mahakama Kuu ya Tanzania? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Waziri mhusika, Mheshimiwa Profesa karibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, Sheria ya *CyberCrime* au Makosa ya Mtandao ni sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria hii inafanya kazi pande zote mbili za Muungano kwa maana ya Zanzibar au Bara. Sheria hii tayari imeshaanza kufanya kazi na tunasimamia maeneo yote ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimuambie Mheshimiwa Rukia kwamba sheria hii ni ya Muungano na imeshapitishwa kwa taratibu zote.

SPIKA: Kwa hiyo Mheshimiwa Dkt. Suleiman ziko sheria zinafanya kazi kote kote, zinakatakata kote kote.

Inafuatiwa Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kingamboni, tafadhalii.

Tatizo la Umeme Kigamboni

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE aliuliza:-

Wilaya ya Kigamboni ina uwekezaji mkubwa katika sekta ya nyumba na viwanda, mahitaji ya umeme kwa sasa ni zaidi MW 20; lakini ni MW 8 tu zinazopatikana, nao umekuwa ukikatika mara kwa mara kutokana na mahitaji makubwa pamoja na uchakavu wa miundombinu ya umeme.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha Kigamboni inapatikana umeme wa uhakika?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha kupoozea umeme (*substation*) katika Wilaya ya Kigamboni kutokana na mahitaji makubwa ya umeme?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*) inakamilisha utekelezaji wa mradi wa uboreshaji umeme katika Jiji la Dar es Salaam kupitia mradi wa *TEDAP*. Mradi huu unahusisha ujenzi wa vituo vya kupooza umeme vya Mbagala na Kurasini. Kazi ya vituo hivyo ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa umeme katika maeneo ya Kigamboni kwa kuwa Kigamboni sasa itakuwa ikipata umeme kutoka katika vituo hivi vya Mbagala na Kurasini badala ya Kipawa na Ilala kama ilipokuwa hapo nyuma. Ujenzi wa mradi huu ulianza mwaka 2012 na utakamilika mwishoni mwa mwezi Septemba, 2017.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kulipatia ufubuzi wa kudumu tatizo la upatikanaji wa umeme eneo la Kigamboni, Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*) linajenga njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Kurasini kwenda Dege – Kigamboni na kujenga kituo cha kupooza umeme chenye uwezo wa kilovoti 132 chenye uwezo wa kufua umeme wa MVA 120 sawa na MW 100. Taratibu za ujenzi zimeanza mwezi Agosti, 2017 na kazi inatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2018. Gharama ya mradi huu inakadiriwa kufikia shilingi bilioni tano.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, swalii la nyongeza.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yanatupa matumaini wananchi wa Kigamboni hususani kwa changamoto ambayo inatukabili. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wilaya ya Kigamboni haikupata miradi mipya na hii inatokana na kwamba miradi ya mwaka jana (2016/2017) haikutekelezwa kikamilifu. Changamoto moja ilikuwa ni hali ya upatikanaji wa vifaa kwa maana ya transfoma, nguzo ndogo pamoja nyaya. Je, Naibu Waziri anaweza akatuhakikishia kwamba katika mwaka huu wa fedha transfoma zaidi ya 30, nyaya kilometra zaidi ya 30 na nguzo takribani 1,000 ambazo tunazihitaji tunaweza tukazipata ili kutekeleza miradi hii?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Kigamboni ililingizwa katika *REA* Awamu ya Pili na kuna vijiji ambavyo vilirukwa. Je, utekelezaji wa *REA* Awamu ya Tatu kwa maeneo ambayo yalibaki unaanza lini?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nichukue nafasi hii kumshukuru

na kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Kigamboni jinsi anavyofuatilia maendeleo ya wananchi wa Kigamboni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na suala la vifaa, kwanza kabisa tukiri kwamba kulikuwa na shida ya upatikanaji wa nguzo, transfoma pamoja miundombinu ya *TANESCO*, lakini kuanzia mwezi Juni kwa niaba ya wananchi wa Kigamboni na Watanzania wengine wote, sasa nguzo zinapatikana hapa nchini na zinatosha kupeleka miundombinu katika maeneo yote. Nitoe tu tamko kwamba katika nchi nzima tulikuwa na wateja 29,000 ambao hawajaunganishiwa umeme wakati wameshalipia kuunganishiwa umeme, lakini wananchi hao wamepelekewa umeme bado wananchi 32 tu. Kigamboni eneo ambalo ni muhimu sana hadi sasa tumepeleka nguzo 2,100 na wateja walliobaki ni 30. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wananchi wako wa Kigamboni Mheshimiwa Ndugulile kule Mwanzo Mgumu tumeshawapelekea nguzo, Msongozi kwa Mpika Chai na Cheka tumeshapeleka nguzo. Kwa hiyo, wananchi wataendelea kuunganishiwa umeme kama kawaida. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na miradi mingine ya Jimbo la Kigamboni, ni kweli kabisa tulipeleka miradi ya *REA* katika vijiji viwili Kigamboni kwa sababu Kigamboni kimsingi ni mitaa kwa sababu ipo Jijini Dar es Salaam, lakini tulipeleka mradi wa *REA* Kisarawe II kwenye eneo la Cheka pamoja na Kimbiji. Tuna mradi mwengine ambao upo chini ya *TANESCO* na umeshaanza ambao utapeleka umeme kwenye vijiji vya Mheshimiwa Ndugulile. Vijiji ambavyo vitapelekewa umeme ni pamoja ni Changanyikeni, Gezaulole pamoja na maeneo yote ya Dege.

Sambamba na hilo, tumepeleka mradi mwengine, kule Kigamboni kulikuwa na transfoma moja yenye uwezo wa MW 5 tu, sasa tumeing'oa tumeweka yenye MW 100 ambayo itapeleka umeme kwenye vijiji vyote vya Kigamboni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimpe tu faraja mhesimiwa Mbunge wa Kigamboni kwamba matatizo ya umeme Kigamboni sasa yanaelekea kuisha. Utekelezaji wa *REA* umeshaanza tangu Juni, 2017 na utakamilika Machi, 2019. (*Makofi*)

SPIKA: Niliwaona Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba na mimi nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, umeme wa *REA* unatarajiwa kuwa ni tegemeo kubwa sana kwa wananchi, lakini pia kuinua uchumi kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo, lakini Kaliua umeme wa *REA* umekuwa unakatika mara kwa mara, Mheshimiwa Waziri nimeshakuja kwako mara nydingi tu kuhusiana na suala hili. Kwa siku zaidi ya masaa nane, masaa manne unawaka, masaa nane hauwaki, kwa hiyo lile tegemeo halipo tena kwa wananchi wale. Mheshimiwa Waziri aliahidi kujenga *substation* pale Kaliua alivyotembelea mwaka 2015.

Naomba kujua sasa Serikali ina mpango mkakati gani kuhakikisha kwamba inajenga *substation* pale Kaliua ili umeme wa *REA* uweze kuwa na tija na kuinua uchumi wa wanachi wa Kaliua? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu umeme Kaliua.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa, Mheshimiwa Sakaya nilipokuja kwako nilitembea na wewe sana na naomba niendelee kutembea na wewe nikija tena. Lakini pia ... (*Kicheko*)

SPIKA: Wewe Msukuma ongea Kiswahili cha Kibunge, najua Wasukuma wana shida sana hawa. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli alivyosema Mheshimiwa Mbunge, umeme unaosafiri kwenda Kaliua ni ule unaotoka Tabora - Urambo, - Kaliua hadi Uvinza, kwa hiyo, ni umbali mrefu sana. (*Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa mtamuua bure ana nia njema tu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Mbunge anavyosema, transforma ya kusafirisha umeme iliyopo Tabora ndiyo inayohusika kusafirisha umeme katika Majimbo ya Kaliua, Urambo mpaka Uvinza, umbali wa kilometra 372. Mkakati madhubuti wa kumaliza tatizo hili la kukatika kwa umeme ni kuwa Serikali sasa inajenga *substation* katikati ya Kaliua pamoja na Urambo katika eneo la Gologolo.

Kwa hiyo, utaratibu umeanza na wakati utekelezaji wa *REA* utakapoanza basi wananchi watapata umeme huo lakini katika jibu langu litakalofuata kwa swali la msingi nitaeleza kwa upana zaidi lakini nimpe uhakika Mheshimiwa Mbunge utaratibu fedha zimeshatengwa na *survey* imekamilika na ujenzi utaanza hivi karibuni.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane jamani, nimeshamuomba Mheshimiwa Profesa Ndalichako, Waziri wa Elimu na amekubali Wasukuma na Wanyamwezi wote mtapata *tuition* ya Kiswahili. Mheshimiwa swali la nyongeza tafadhali. (*Kicheko*)

MHE. DESTERY B. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na hasa niendelee kuanidka Kiswaga. Kwa kuwa swali langu linafanana kabisa na suala hili la Kigamboni, Wilaya ya Magu ambayo ni Jimbo lina vijiji 82, ni vijiji 29 tu vina umeme. Je, vijiji 53 ni lini vitapatiwa umeme ambavyo hata Mheshimiwa Dkt. Kalemani anavifahamu? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Dkt. Kalemani, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimsahihishe kidogo Mheshimiwa Kiswaga, vijiji ambavyo havijapata umeme katika Jimbo la Magu siyo 53 vipo 56. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kiswaga tutakupelekea umeme.

Mheshimiwa Spika, niseme tu utekelezaji wa *REA* Awamu ya Tatu umeshaanza na katika Wilaya yake, maeneo yote yameshafanyiwa *survey* na Mheshimiwa Mbunge tumeenda naye na tumetembelea maeneo hayo na nimhakikishie vile Vijiji vya Mahala, Igombe, Shishani, Nyasato, Kayera mpaka Mahala vitapatiwa umeme na utekelezaji huo umeshaanza. Nikupe tu uhakika kwamba *survey* itakamilika tarehe 10 mwezi huu na wakandarasi wataanza kazi rasmi. Kama nilivyosema tuliboresha kwa sababu vile vijiji vyako vitatu vimepelekewa nguzo moja moja kwa hiyo sisi tunahesabu kama vijiji vyote havijapata umeme, kwa hiyo, ni 56 katika Jimbo la Magu.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, baada ya kutoka Kaliua sasa tupo Urambo.

Na. 9

Tatizo la Kukatika kwa Umeme Uendao Urambo

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza:-

Wilaya ya Urambo inapokea umeme kutoka kwenye kituo cha kupoozea umeme cha Kaloleni umbali wa kilometra 90 kufika Urambo ambako ndiko kiliko kikata umeme inapokuwa kumetokea tatizo katika njia. Aidha, chanzo hicho cha umeme pia kimetegemewa na Wilaya ya Kaliua, Jimbo la Ulyankulu na vijiji vya Ikomwa, Igange, Tumbi, Ilolangulu hadi Ugoola (Tabora na Uyui); uzoefu unaonyesha kwamba kama kukitokea tatizo la kiufundi katika njia huwa inasababisha kukatika kwa umeme katika njia nzima likiwemo Jimbo la Urambo na kusababisha malalamiko mengi kwa *TANESCO*.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Je, kwa nini Serikali isijenge kituo cha kupoozea umeme (*substation*) karibu na Wilaya ya Urambo ili kiweze kutoa umeme wa uhakika katika Wilaya hiyo inayozidi kukua katika mahitaji ya umeme hasa katika kutekeleza sera ya viwanda na katika taasisi zinazotoa huduma za kijamii kama hospitali, shule na kadhalika kwenye Jimbo hilo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea kuimarisha upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Tabora na Kigoma kwa kujenga njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 133 yenye urefu wa kilometra 372 kutoka Tabora kupitia Urambo, Kaliua, Uvinza na hatimaye Kigoma.

Mheshimiwa Spika, katika mradi huu, kituo cha kupoza umeme (*substation*) cha kilovoti 132 kitajengwa kati ya Urambo na Kaliua kitakachosafirisha umeme katika Wilaya ya Urambo, Kaliua, Uvinza hadi Kigoma na hivyo kuimarisha miundombinu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu wa mradi huu ulianza mwezi Juni, 2017 na utakamilika mwezi Septemba, 2017. Ujenzi rasmi wa mradi unatarajiwa kuanzia mwezi Aprili, 2018 na kukamilika mwezi Agosti, 2018. Mradi huu utagharimu shilingi bilioni 179.

SPIKA: Mheshimiwa Mama Margaret Simwanza Sitta.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza, kama ifuatavyo:-

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu zuri pamoja na Serikali kwa ujumla kwa kukubali ombi letu la wananchi wa Urambo la kujenga kituo cha kupoza umeme (*substation*) Wilayani kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza linasema, je, Serikali inaweza kuwahakikishia wananchi wa Urambo kwamba katika Awamu ya Tatu ya REA vijiji vyote veya Wilaya ya Urambo vitapata umeme? (*Makofii*)

SPIKA: Swali fupi, majibu mafupi Mheshimiwa Dkt. Kalemani, vijiji vyote.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpengeza Mheshimiwa Margaret Sitta kwa juhudii kubwa anazofanya kufuatilia maendeleo ya wananchi wa Urambo, hongera sana Mheshimiwa Sitta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba ni kweli vijiji vyote 27 vilivybaki katika Jimbo la Urambo vitapata umeme ikiwemo Yerayera, Igembesabo, Ifuta na vijiji vingine. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimu muda, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, swali linaulizwa na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo.

Na. 10

Kudhibiti Nyani Waharibifu wa Mazao – Rombo

MHE. JOSEPH R. SELASINI aliuliza:-

Kumekuwa na usumbufu na uharibifu unaosababishwa na ongezeko la nyani ambao wanavamia mashamba ya wananchi na kula mazao kama mahindi, ndizi na sasa wanaingia katika majumba ya watu na kubeba chakula katika Kata za Ushiiri, Mrao – Keryo, Kirua – Kei, Katangera – Mrere, Kirongo – Samanga na Olele.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapunguza au kuwahamisha nyani kwenye maeneo hayo?

(b) Je, kuna utaratibu gani wa kuwafidia wananchi hasara waliyoipata kutokana na uharibifu wa nyani hao?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Injinia Ramo Makani, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii inatambua uwepo wa tatizo la wanyamapori wasumbufu na waharibifu ambao wanaharibu mazao katika kata zilizotajwa ambazo zinapakana na Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro. Wizara kuititia Taasisi yake ya *TAWIRI* imepanga kuendesha zoezi la utafiti wa wanyamapori aina ya nyani, ngedere na kima katika kipindi cha mwezi Oktoba hadi Disemba 2017 ili kubaini idadi na mienendo yao na kuwianisha na shughuli za kilimo zinazofanyiwa na wananchi katika maeneo ya vijiji vyta kata zilizotajwa. Kwa sasa Wizara imeandaa utaratibu wa kushirikisha jamii husika katika kulinda mazao yao kwa kutumia mbinu mbalimbali za kitaalam na za kijadi, hatua ambayo itatekelezwa kuanzia mwezi Oktoba 2017 kwa Wizara kuwashauri wananchi kuanzisha vikundi, kuendesha mafunzo na kuwapatia silaha za jadi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufidia hasara, kwa sasa Serikali haina utaratibu wa kufidia mazao yaliyoharibiwa au kuliwa na wanyamapori na badala yake Kanuni za *Dangerous Animals Damage Consolation* za mwaka 2011 chini ya Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009 zinaelekeza ulipaji wa kifuta jasho. Hata hivyo, katika kanuni hizo, jamii ya nyani siyo mionganoni mwa wanyama wanaotambulika kisheria katika ulipaji wa kifuta jasho. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Selasini, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza Waswahili wana msemo kwamba ukitaka kujua utamu wa ngoma uingie ucheze. Tatizo hili ni kubwa sana na binafsi nilikwishaongea na Naibu Waziri akawa ameniahidi atanipelekea mtaalam kutoka Arusha, hili siyo tatizo la mwaka huu nashangaa jibu linasema kwamba wanaanza kufanya utafiti. Wale wanyama wanaendelea kuzaliana, wanaendelea kuleta usumbu, sasa hivi wanaingia hata ndani wanaepua chakula kikiwa jikoni na ni hatari sana kwa akina mama na nikisema ni hatari kwa akina mama nadhani kila mtu anaelewa. Sasa nataka nijue huu utafiti utakwisha lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, miaka ya nyuma nyani hawa walikuwa wanadhibitiwa na wananchi wenyewe kwa kuwaua kwa risasi ambazo zilikuwa zinagawiwa kutoka kwenye Ofisi ya Maliasili lakini sasa hivi wamekatazwa kufanya hivyo na Maliasili hawa hawa. Sasa naomba niulize Wizara, kwa kuwa imetamka kwamba inakusudia kuwashirikisha wananchi kwa kutumia silaha za jadi, je, Wizara iko tayari wananchi wenyewe silaha kama magobole na kadhalika watumie risasi kama utaratibu wa zamani? Mimi Mbunge wao niko tayari kuwanunulia risasi ili tupambane na hawa wanyama vinginevyo watuletee Wa-Congoman waje wawale kule na siyo kutuambia utafiti wakati wanaharibu watu. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, ingawaje tunajuliza huko Rombo mbona hawalalamikii nyati na nini, analalamikiwa nyani tu?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza Wizara kwa niaba ya Serikali inawapa pole wananchi wa maeneo ya kata zilizotajwa kutohana na

usumbufu huo wa wanyama hawa nyani na ngedere na uharibifu wanaosababisha kwenye mashamba yao. Kwenye swali lake la kwanza la nyongeza anauliza utafiti utaisha lini, kwenye jibu la msingi nimesema utafiti huo unakamilika mwezi Disemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa nini tunafanya utafiti wakati ni dhahiri kwamba wanyama wapo na wanasumbua na wanaharibu. Mimi nafikiri utafiti ndiyo njia nzuri ya kuweza kufika mahali kupata jibu au suluhisho. Ni sawasawa na mtu anayeumwa malaria ambaye hataki damu itolewe iende kwanza ikapimwe, nafikiri hiyo haitakuwa njia sahihi. Nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumedhamiria na tunakusudia na mimi na wewe tunaweza tukapata nafasi kabisa kupeana taarifa ya mara kwa mara katika kipindi hiki kabla ya hiyo Disemba ili tuweze kuona tunasonga mbele namna gani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya silaha, matumizi haya yapo kwa mujibu wa sheria na kama ni matumizi ya risasi za moto sheria zinakuwa kali zaidi. Katika eneo hilo hao Serikali inashughulikia masuala hayo kwa kushirikisha Wizara zaidi ya moja, si suala la Wizara ya Maliasili na Utalii tu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba utafiti sasa ndiyo unaweza ukatuwezesha tuone ukubwa wa tatizo, uzito wake, kama utaainisha kwamba matumizi ya silaha za moto ni lazima basi labda tunaweza tukaenda huko kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo lakini kama kwenye utafiti tukiona tunaweza kutumia njia nyingine ambayo siyo silaha za moto basi itakuwa ni vema tutumie njia hizo ambazo tutazipata.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali kwa sababu ya muda. Kuna Mbunge mmoja wa upande wangu wa kulia ameniandikia hapa anahitaji maelezo ya haraka kuhusu jambo linaloendelea hapa ndani ya ukumbi. Anasema Mheshimiwa Spika, ni kwa nini wenzetu wengine leo wamevaa nguo nyeusi humu ukumbini? (*Makof!*)

Sasa anasema au wanaomboleza kutokana na kufutwa kwa matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa nchi jirani? Nikasema kwa kweli sijui kama ni hivyo lakini tukiwaauliza wao wenyewe wanawenza wakasema uchaguzi huo kwani unahusiana nini na sisi? (*Makofi/Kicheko*)

Tunaendelea na maswali Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala.

Na. 11

Msitu wa Hifadhi ya Taifa Minziro

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA aliuliza:-

Msitu wa Hifadhi ya Taifa Minziro una vivutio vingi vya utalii.

(a) Je, ni watalii wangapi wametembelea msitu huo ndani ya kipindi cha miaka 20 hadi sasa?

(b) Je, wananchi wanaoishi karibu na msitu huo wananaufaikaje?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tuko Wizara ya Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya mwaka 2015, Msitu wa Hifadhi wa Minziro haukuwa mionganoni mwa maeneo yaliyohifadhiwa na kusimamiwa kwa ajili ya shughuli za utalii. Hata hivyo, kwa sasa hifadhi hiyo ipo katika hatua za awali za maandalizi ya mpango endelevu wa kuendesha utalii wa ikolojia katika msitu huo.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015 Serikali ilianzisha mradi wa kuboresha uhifadhi wa bionuwai katika hifadhi 12 za misitu ya mazingira asilia zilizopo nchini. Hifadhi hizo zikiwa ni pamoja na Mlima Rungwe kule Mbeya, Udzungwa na Kilombero zinazopakana na Iringa na Morogoro, Uluguru na Mkingu zinazopakana na Morogoro, Amani, Nilo na Magamba zilizopo ndani ya Mkoa wa Tanga, Chome kule Kilimanjaro, Rondo – Lindi na Mlima Hanang Mkoa wa Manyara, chini ya mradi unaofadhiliwa na Mfuko wa Mazingira na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*). Aidha, kutokana na kuwepo kwa mipango ya awali ya kuanzisha utalii wa ikolojia katika hifadhi hiyo, katika kipindi cha mwaka 2014 hadi 2015 jumla ya watalii 11 walitembelea hifadhi hiyo ambapo tisa ni raia wa kigeni na wawili ni Watanzania.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaoishi jirani na Misitu wa Minziro kwa kutunza, kuhifadhi na kulinda msitu huu kwa sasa wananzaika kwa kupata vyanzo bora vya maji, hali ya hewa iliyo bora na ardhi yenye rutuba na sifa nyaginezo muhimu kwa kilimo na maisha ya wananchi kwa ujumla. Aidha, katika siku zijazo baada ya kukamilika kwa mpango unaoandaliwa na Wakala wa Huduma za Misitu, wananchi hao wananzaika kwa kupata gawio la asilimia 26 ya mapato yatakayotokana na utalii wa ikolojia ambao hufanyika kwa njia shirkishi na wananchi katika kusimamia hifadhi na kuendesha utalii huo.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kamala, swali la nyongeza.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, huo mpango unaoandaliwa ni jambo jema na kwa kuwa mpango huo utatusaidia vijiji vinavyozunguka maeneo hayo kupata asilimia 26, ni lini maandalizi ya mpango huo yatakamilika? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa katika kata hiyo ulipo Msitu wa Minziro kuna kitongoji kinaitwa Bulembe na kwa kuwa katika kijiji hicho kuna ngome zilizotumiwa na Wajerumani kupigana Vita ya Pili ya Dunia na kwa kuwa katika eneo hilo huwezi kwenda kwa sababu hakuna barabara isipokuwa uwe jasiri kutumia pipipiki au kutembea kwa miguu zaidi ya saa sita, je, Waziri au Naibu Waziri yuko tayari kuandamana nami kutembea zaidi ya saa sita kwenda kuona vivutio hivyo? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu kwa ufupi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umesema kwa ufupi ni kwa ufupi kwa sababu na maswali yenye kila yanaelekeza kupata majibu kwa ufupi. Kuhusu swalii lake la kwanza, lini mpango utakamilika, mpango huu utakamilika ndani ya mwaka wa fedha uliokwishaanza.

Mheshimiwa Spika, swalii lake la pili, je, Waziri au Naibu Waziri yuko tayari kuandamana naye kwenda kuona vivutio alivyovitaja ambavyo viko ndani ya msitu lakini pia ni vivutio vya malikale.

Mheshimiwa Spika, jibu lake ni kwamba mimi au Mheshimiwa Waziri wakati wowote ule tutakapokuwa tumepata fursa na hasa baada ya kikao hiki cha Bunge tutakuwa tayari kwenda kuona na tutaweza kuona namna gani tunaweza tukaondoa changamoto hiyo ya miundombinu ambayo ni mojawapo ya changamoto zinazosumbua kwenye sekta ya utalii.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Tunaongeza muda kidogo maana tumeanza nusu saa baada kutokana na zoezi tuliloanza nalo leo asubuhi ili tumalizie haya maswali. Swalii la Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 12

Kujenga Upya Kituo cha Polisi Dunga

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA aliuliza:-

Kituo cha Polisi Dunga kimechakaa sana kwani kuta zake zimepasuka na baadhi ya vyumba havitumiki kutokana na kuhatarisha usalama wa askari na wananchi wanaofika kwa ajili ya kupata huduma.

Je, ni lini Serikali itajenga upya kituo hicho?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na Kituo cha Polisi Dunga pamoja na Wilaya zote mpya zilizoanzishwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Kwa kutambua umuhimu wa Kituo cha Polisi Dunga, tathmini itafanyika ili gharama halisi ziweze kujulikana. Aidha, ujenzi wa kituo hicho utaanza mara baada ya fedha kupatikana kwa ajili ya kipaumbele cha Serikali na hivi sasa katika kukamilisha miradi ya zamani ya polisi na kuanza miradi mipyä ya ujenzi wa vituo hivyo nya polisi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali kuimarisha miundombinu ya ulinzi na usalama, tunatoa wito kwa wadau mbalimbali wa maendeleo kushiriki katika ujenzi wa vituo nya polisi ili huduma za ulinzi na usalma ziweze kupatikana kwa karibu.

SPIKA: Mheshimiwa Asha.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu yenyeye kutia moyo ya Mheshimiwa Waziri, hivi anafahamu kituo hiki sasa hivi kimefunga huduma zake na wanatoa huduma kwenye jengo la kuazima? Je, ni lini tathmini hii itafanyika ili gharama ijulikane na umuhimu wa kukijenga pia uonekane? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia anawahakikishia vipi wananchi wanaotumia kituo hiki umuhimu wa kujengwa na kuweza kuitumia kama walivoyozoea? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, mama yangu Asha, kwa kweli kwa kufuatilia sana suala la kituo hiki. Mbali na swali la hapa amekuwa pia akiulizia mara zote anapopata fursa ya kutembelea ofisini ama kwenye shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, niseme tu, kwa umuhimu huo na kwa ufuatilaji wake, jambo hili tumesema lifanyiwe tathmini kwa upekee kwa maana ya Kituo cha Dunga kama kituo peke yake mbali ya vituo vingine kwenye maeneo mengine ambavyo vinafanana kama kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, mara tathmini hiyo itakapokuwa imekamilika ambapo tunaamini ni katika kipindi hikihiki, basi utaratibu wa upatikanaji wa fedha utaanza na hapo ndipo tunaposema tunatoa rai hata kwa wadau mbalimbali ili tuweze kufanya kama ni jambo mahsus kufuatana na mazingira ya pale.

Mheshimiwa Spika, mara ukarabati wake utakapokamilika basi niwahakikishie wananchi kwamba matumizi yake yatarejea katika hali ya kawaida na wataendelea kumpongeza na kumpigia kura Mheshimiwa Mbunge ambaye amelitetea sana jambo hili. (*Makofi*)

SPIKA: Kwa kifupi twende Pemba, swali la nyongeza Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nina swali moja tu dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu hapa Bungeni Serikali imekuwa ikiahidi kikitengeneza Kituo cha Polisi cha Kengeja ambacho ni kibovu, chakavu na cha zamani ambacho mnasema mlirithi kutoka kwa wakoloni lakini mara nyingi hamkitengenezi na kimekuwa kikihatarisha maisha ya askari na baadhi ya wale wanaowekwa pale kwa muda.

Je, ni lini Serikali hasa itaandaa mazingira ya ziada kuhakikisha mnakikarabati kituo hiki ili kuепusha madhara yanayoweza kutokea? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo la nyongeza, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Mjumbe makini wa Kamati inayosimamia Wizara ya Mambo ya Ndani, naye nimhakikishie tu kwamba kikosi chetu kinachosimamia masuala ya ukarabati kitafanya tathmini pamoja na kituo anachokiongelea.

Mheshimiwa Spika, ni kipaumbele cha Wizara kufanya ukarabati na kukamilisha majengo ya vituo ambavyo vimeshafikia hatua za kuweza kutumika ili vianze kutumika na cha kwake tutaweka umuhimu huo kama alivyo hitaji kwenye swali.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Swali la Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini.

Mfumo wa Usambazaji Maji Kutoka Visima Virefu Jimbo la Singida Kaskazini

MHE. LAZARO S. NYALANDU aliuliza:-

Vijiji vyote vya Tarafa ya Ilongero, Mtinko na Mgori bado vinahitaji mfumo wa usambazaji maji kutoka visima virefu vilivyopo kwenye baadhi ya vijiji na tarafa hizo tatu zinahitaji kuongezewa visima virefu na mabwawa ya kuhifadhia maji ya mvua.

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanikisha mradi huo ili kuwaondolea adha wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Naibu Waziri Kamwelwe.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Singida inaendelea kushirikiana na washirika mbalimbali wa maendeleo katika kuhakikisha huduma ya maji inapatikana. Hadi sasa wananchi wanaopata huduma ya maji kwa Halmashauri ni asilimia 53 sawa na wakazi 130,908.

Mheshimiwa Spika, katika Tarafa ya Ilongero kuna miradi 24, Tarafa ya Mtinko kuna miradi 14 na Tarafa ya Mgori kuna miradi kumi iliyokamilika na inatoa huduma ya maji. Miradi mingi kati ya hii inatumia nguvu ya nishati ya jua kuendesha mitambo ambayo imeunganishwa moja kwa moja kwenye chanzo au kisima na kujengewa kituo kimoja cha kuchotea maji.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri imeanza kufanya upanuzi wa miundombinu ya maji katika kijiji cha Pohama, Tarafa ya Mgori, ambao umeflikia asilimia 90 ya utekelezaji. Halmashauri inaendelea kufanya usanifu wa miradi ya maji kwa ajili ya ujenzi wa mitandao ya mabomba kutoka kwenye visima katika vijiji vya Mtinko na Ghalunyangu, Tarafa ya Mtinko na Ngamu, Tarafa ya Iliongero. Aidha, ujenzi wa miradi hiyo unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Halmashauri imepanga kuchimba visima virefu na kujenga mitandao ya mabomba katika vijiji 11 na vijiji hivyo ni pamoja na Merya, Mughamo, Mughunga, Msange, Itaja, Mudida, Ughandi, Kijota, Mwasauya, Mtinko na Mwakiti. Pia kufanya ukarabati na upanuzi wa miradi katika Viji vya Msange, Ghalunyangu, Ngimu, Mdilu, Mwasauya, Pohama, Nkwae, Msisi na Sagara.

SPIKA: Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, tunakushukuru sana kwa watoto wa Arusha ambao wamerudi salama nchini. Ahsante sana kipekee Mheshimiwa. Swali la nyongeza, tafadhalii. (*Makofii*)

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na kwa kweli Serikali nzima, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa wanavyoshughulikia suala zima la maji katika maeneo ya vijiji tunavyotoka. Nawashukuru sana kwa niaba ya wananchi wangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nitoe ombi la pekee, wananchi wa Tarafa ya Mtinko na Mji Mdogo wa Mtinko ambao ni mji unaokuwa kwa kasi sana na una watu wengi. Mfumo wao wa maji ulitegemea kuwepo na pampu iliyoharibika na hapa tunavyozungumza kuna dharura kubwa sana ya maji katika Mji huu Mdogo wa Mtinko. Naomba kwa kadri inavyowezekana Serikali iangalie uwezekano wa haraka wa kuweza kusaidia tatizo hili la Mtinko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe*, maji Mtinko.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ameipongeza Serikali kwa kutekeleza miradi ya maji hapa nchini, Mheshimiwa Nyalandu nakushukuru sana lakini pia na mimi nakupongeza wewe kwa sababu juhudhi kubwa umeifanya katika Jimbo lako. Pamoja na Serikali kuwa na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji lakini wewe mwenyewe binafsi umekuwa unawasiliana na wafadhili ndiyo maana jimbo lako limefikia katika hatua hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ombi lako la pumpu tunalichukua na nakuomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane leo leo, tushirikiane pamoja na Mkurugenzi hili ni tatizo dogo ili tuhakikishe pumpu hii inapatikana kwa haraka ili wananchi wa Mtinko wapate maji

SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

Na.14

Ukatili wa Watumishi wa Majumbani Nchi za Kiarabu

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA aliuliza:-

Watanzania wengi hasa wanawake wanaokwenda kufanya kazi za ndani katika nchi za kiarabu kama Oman na nyinginezo wamekuwa wakifanyiwa ukatili mkubwa sana unaosababisha wengine kufariki na wengine kujeruhiwa vikali.

(a)Je, Serikali ina utaratibu gani madhubuti wa kudhibiti safari za Watanzania hao wanaokwenda katika nchi

za Kiarabu na pia kuwabana Mawakala na kuwajibisha inapobidi?

(b)Je, ni wanawake wangapi wa Kitanzania wameuawa katika Nchi za Kiarabu na fidia kutolewa katika familia zao?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu mzuri wa kutoa vibali kuititia mamlaka zinazoshughulikia masuala ya ajira ikiwemo Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (*TAESA*) iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu inayoshughulikia masuala ya kazi, vijana, ajira na watu wenye ulemavu kwa kushirikiana na Wizara inayoshughulikia masuala ya kazi Zanzibar na Balozi zetu zilizoko nchi mbalimbali huko Mashariki ya Kati.

Serikali imeweka miongozo itakayosaidia siyo tu kuwabana mawakala bali pia kuwasaidia Watanzania kutumia fursa za ajira zilizopo nje ya nchi ili kupunguza tatizo la ajira hasa kwa vijana kwa kuelekeza kila mfanyakazi kuwa na wakala rasmi na kupata mkataba kutoka Ubalozi.

Mheshimiwa Spika, Ubalozi unakuwa na taarifa katika kila hatua ambayo Watanzania wanapitia wakati wa maandalizi ya kwenda kufanya kazi hivyo kulinda maslahi yao. Aidha, mwajiri anayetaka kuajiri wafanyakazi kutoka Tanzania atatakiwa kusoma na kuelewa mwongozo na

baada ya kukubaliana nao anatakiwa kujaza fomu ya kuomba kumwajiri Mtanzania na kuwasilisha Ubalozini kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Maombi hayo yatafuatiwa na mkataba wa kazi.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu una vupengele vikuu vitano ambavyo mwajiri na mawakala wanapaswa kukidhi mahitaji yake ili Serikali itoe idhini kwa Mtanzania aliye tayari kufanya kazi aendelee na taratibu za ajira katika nchi hizo. Vipengele hivyo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Taarifa za mwajiri.
- (ii) Taarifa za mwajiriwa.
- (iii) Mshahra wa mwajiriwa.
- (iv) Masharti ya mkataba.
- (v) Maelezo ya mawakala wa Tanzania na Oman.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa Watanzania zaidi ya 12,000 ambaa Balozi unawatambua wanafanya kazi katika kada mbalimbali nchini Oman. Kati ya hao, wanawake watatu wamepoteza maisha kwa sababu mbalimbali ikiwemo ugonjwa, ajali na kadhalika. Katika vifo vilivyowahi kuripotiwa ambapo Serikali ilifuatilia hadi kujua vyanzo halisi vya vifo hivyo, hakuna taarifa kuhusu vifo vilivyosababishwa na mauaji ya makusudi.

Aidha, mara zote tunapopata taarifa za vifo katika nchi hizo, Serikali huchukua jukumu la kufuutilia kwa kushirikiana na mamlaka za nchi husika kujua hatma za familia zilizopoteza mwenzi wao ikiwa ni pamoja na malipo ya fidia kutoka kwa mwajiri wa marehemu.

Mheshimiwa Spika, wakati wote Serikali imekuwa makini katika hatua za awali za maandalizi ya safari hizo kwa kuwabana mawakala na kuhakikisha kuwa mikataba inakuwa ni mizuri ili kuwezesha kuziba mianya yote ya kukwepa majukumu kwa pande zote inayoweza kusababisha Watanzania wanaokwenda kufanya kazi katika nchi hizo kupoteza haki zao.

SPIKA: Mheshimiwa Asha ameridhika, swali la nyongeza.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nashukuru kwa majibu, nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa pamoja na mikataba na vipengele vingi vilivyoratibiwa vizuri hali bado kwenye eneo hili siyo nzuri. Bado wananchi wetu wengi wanaendelea kupata matatizo hasa wanawake wanaokwenda kufanya kazi nchi za Urabuni. Serikali kuitia Ubalozi wetu inalazimika kutumia gharama nyingi za kifedha ambazo zingeweza kutumika katika shughuli za maendeleo, kwa mfano, miundombinu, *standard gauge* na kutununulia ndege nyingine ya *Bombadier*. Je, Serikali haijaona kwamba sasa wakati umefika wa kuwakatibisha hawa *ma-agent*, wafanya mikataba ili kuweza kuweka *deposit* ya fedha ambazo zitatumika kuwashughulikia wananchi wetu hawa inapobidi kurudishwa wanapokuwa wagonjwa wakati wanapokuwa wametelekezwa na waajiri wao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa zipo taarifa na malalamiko kwamba baadhi ya wananchi wetu hawa wanaokwenda kufanya kazi huko huambiwa, kwa mfano, wanakwenda kuuza duka wakafika kule wakafanyishwa kazi nyingine kinyume na hilo duka na kinyume na ridhaa yao na pengine kusababisha hatari kwenye afya zao. Je, Serikali inalisaidiaje jambo hili katika kudhibiti na kuhakikisha kama wananchi wetu hawaendi kuongezewa udhalilishaji huko nchi za Kiarabu? Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Asha, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI): Mheshimiwa Spika, la kwanza, Mheshimiwa Mbunge alitaka kujua namna ambavyo Serikali tutaweka mfumo mzuri wa kuweza kuwabana mawakala

hawa. Kazi hii ya kuwapeleka Watanzania kufanya kazi nje ya nchi inaratibiwa kwa mujibu wa sheria zetu na mawakala hawa wanajasiliwa katika utaratibu ambao umewekwa. Wakala yejote ambaye anavunja masharti na matakwa ya sheria hizi tumekuwa tukimchukulia hatua kwa kufuta pia usajili wake ili kumtaka ufuate taratibu za nchi ambazo tumeziweka katika kupeleka wafanyakazi nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika eneo hili nitoe rai tu kwa wafanyakazi wote ambao wanafanya kazi nje ya Tanzania hasa katika nchi za Kiarabu hususani Oman kufuata taratibu tulizoziweka kupitia Ofisi ya Wakala wetu wa Huduma za Ajira (*TAESA*) ambapo tumeweke utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba kabla ya mfanyakazi wa Tanzania hajatoka nje ya nchi tunafanya kwanza mawasiliano kufahamu kazi anayokwenda kufanya lakini na mkataba na malipo yake. Matatizo mengi yanakuja kwa sababu asilimia kubwa ya wanaokwenda kufanya kazi nje ya nchi hawapitii katika utaratibu ambao tumeuweka na ndiyo maana wakipata matatizo huwa inakuwa ngumu sana kuweza kushughulikia kwa sababu hawajapitia katika mfumo wetu na hawapo katika kanzidata yetu ya watumishi ambao wanafanyakazi nje ya nchi. Nitoe rai kwa Watanzania wote wanaokwenda kufanya kazi nje ya nchi kufuata taratibu ili wapatapo matatizo iwe rahisi kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, katika hili eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelizungumza kuhusu kwenda kufanyishwa kazi kinyume na utaratibu uliowekwa, haya yote yanatokana na iwapo tu wafanyakazi hawa hawatakuwa wamepitia katika ofisi zetu. Sisi tunawabana mawakala ili waje na mikataba ambayo tutaitiwa wote kwa pamoja na Ubalozi utabaki na nakala yake ili kuweza kufuatilia. Inapotokea Mtanzania anafanya kazi tofauti na ile ambayo ilisemwa katika mkataba ni rahisi kwenda kuripoti katika Balozi zetu na sisi kuweza kuchukua hatua.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu sijui lakini ni maoni yangu kwamba hii kitu ya mabinti zetu wadogo kabisa kwenda kufanyishwa kazi za ndani huko ni kurudisha watu

kwenye utumwa tu kwa kweli, hili ni la kuliangalia vizuri sana.
(*Makofii*)

Niliwahi kuviona vile vibinti pale *airport* yaani hata havijui vinakwenda wapi, vinakwenda kufanya nini, kuna haja ya ku-revisitsuala hili. Baadhi yao wanakwenda kupata shida za ajabu sana kule. Kwa hiyo, Serikali ni vizuri ikaliangalia kidogo kama kuna ulazima wa kufanya hivyo kweli. (*Makofii*)

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvumi kwa swali la mwisho la Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali, Mbunge wa Kilombero.

Na.15

Kiwanda cha Sukari Illovo Kuhodhi Upimaji wa Miwa

MHE. PETER A. LIJUALIKALI aliuliza:-

Wakulima wa miwa kata za Sanje, *Msolwa Station*, Kidatu na Mkula wanaouza miwa kwa Kiwanda cha Sukari Illovo wamekuwa wakilalamika kuhusu upimaji wa uzito wa miwa na kiwango cha sukari katika muwa.

Aidha, Kiwanda cha Illovo kimehodhi upimaji wa uzito wa kiwango cha sukari na kisha kuwashurutisha wakulima kuamini kuwa vipimo vyao ni sahihi.

(a)Je, Serikali haioni kuwa utaratibu huu unatoa mwanya kwa wakulima kunyonywa na kupewa vipimo batili?

(b)Je, Serikali haioni kuwa hali hii ya kumuachia mwekezaji kuhodhi upimaji wa uzito na kiwango cha sukari katika muwa hutoa mwanya kwa mwekezaji kumnyonya mkulima?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Peter Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvu, napenda kujibu swalii ya Mheshimiwa Peter Lijualikali, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, upimaji wa uzito wa miwa ya wakulima unaotumiwa na wakulima wa Kiwanda cha Kilombero unatumia mizani maalum (*weighbridge*) ambayo inaratibiwa kwa mfumo wa *computer*. Mizani hiyo huhakikiwa na Wakala wa Vipimo kabla ya msimu wa uzalishaji wa sukari kuanza. Hivyo, kutokana na taratibu hizo hatutarajii mizani hiyo kutoa vipimo batili.

(b) Mheshimiwa Spika, upimaji wa kiasi cha sukari katika miwa hufanyika katika maabara zilizopo kiwandani. Kiwanda cha Kilombero kinafanya upimaji huo kwa uwazi na kimewaruhusu wakulima kuweka wawakilishi wao katika maabara hizo ili kuona na kuhakiki namna ambavyo upimaji unafanyika. Wakulima pia wamewekewa wawakilishi wao katika eneo la kupokelea miwa kabla ya kupimwa na kuingizwa kiwandani ili kuhakikisha kuwa miwa yao inaingia kiwandani na miwa ya kiwanda kwa uwiano ulio sawa.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia changamoto ya kutokuaminiana baina ya pande hizo mbili, Serikali kuitia Bodi ya Sukari Tanzania inafanya ufuatiliaji katika viwanda ikiwemo Kiwanda cha Kilombero ili kuona namna ya miwa ya wakulima na ya kiwanda inavyopimwa katika mizani na upimaji wa kiasi cha sukari katika maabara. Katika msimu wa mwaka 2016/2017 zoezi hilo limefanyika katika Kiwanda cha Kilombero na kuonyesha kuwa upimaji wa miwa pamoja na kiasi cha sukari katika miwa unafanyika kwa uwazi na kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

SPIKA: Ahsante sana kwa majibu mazuri Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri. Mheshimiwa Lijualikali.

MHE. PETER A. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mheshimiwa Waziri mimi ndiyo Mbunge wa Kilombero ambaye naishi Kilombero. Naomba tu nikuambie kwamba haya majibu yako uliyonipa siyo ya kweli. Hakuna mwakilishi anayekaa kiwandani anayetoka upande wa wananchi, ni kiwanda chenyewe kinapima, wananchi wanapewa majibu kwamba *SACCOS*yenu ni hii hapa. Sasa haya majibu Waziri uliyonipa nikuambie siyo ya kweli. Naomba wewe uniambie, mimi kama Mbunge nasema haya siyo ya kweli, wewe haya umeyapata wapi? (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha, hili la mwisho siyo swalii kwa sababu Waziri majibu anayoyatoa ni majibu ya Serikali, kama kuna hoja nyininge basi mtawasiliana huko kwa wakati wenu.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

SPIKA: Nitapokea tu wala msiwe na wasiwasi leo tuna muda wa kutosha maana baada ya hapa tunakwenda kwenye Kamati tu.

Nina matangazo machache lakini nianze na kumpongeza Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Giga, leo ni *birthday* yake. Anatiniza miaka mingapi vile, miaka 15? Basi siri yake, mnaotaka kujua umri wake basi mtamuuliza kwenye chai huko lakini leo ni *birthday* yake, hongera sana Mheshimiwa Najma. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni walioko Jukwaa la Spika bado sijapata vizuri, ila wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambaao wanatoka *British Council* Mkoa wa Dar es Salaam, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wengine mlioko kwenye *gallery* ya Spika, nitaweza kuwatambulisha baadaye kidogo nitakapopata majina yenu na yule ambaye nimemtuma naomba arudi haraka sana alete hayo majina.

Wageni wengine ni ndugu, rafiki na jamaa kutoka mikoa mbalimbali nchini waliokuja kushuhudia kuapishwa kwa Wabunge wapya leo, wageni hao ni 150. Naomba wote pale mlipo mliokuja kushuhudia uapishwaji huu msimame pale pale mlipo. Karibuni sana wageni wetu, najua mmetoka mikoa mbalimbali kuja hapa Bungeni, tumewapokea Wabunge wetu wapya, tutawapa kila aina ya ushirikiano, tuna hakika watafanya kazi nzuri, muendelee kuwaombea kule mlipo, ahsanteni sana. (*Makof*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Maulid Mtulia ambao ni viongozi wa CUF kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. Ahsanteni sana, karibuni sana Dodoma pia. (*Makof*)

Tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa ibada hapa Bungeni, anaomba Waheshimiwa Wabunge wote itakapofika saa 7.00 mchana kutakuwa na ibada pale ghorofa ya pili, Jengo la Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria. Mnajjua wenyewe saa 7.00 mchana mkutane pale kwenye ukumbi wenu wa maombi pale Msekwa, ghorofa ya pili.

Kuna Mheshimiwa Dkt. Andrew Waja na mke wake pale *gallery* ya Spika, hawa ni wageni wangu na Katibu wa Bunge pia, tunawakaribisheni sana, karibuni sana. (*Makof*)

Mwisho, ngoja nione kwanza mambo yalivyo hapa, ni taarifa yangu fupi tu kwamba kwa niaba yenu kama mlivyokwishaarifiwa jana nimekuwa nikifanya juhudzi za kuwa na mahusiano na baadhi ya Mabunge na baadhi ya Mabunge yamekuwa yakiomba kuwa na mahusiano nasi na tumekuwa tukiandikiana *MoU* na baadhi yake ikiwa ni pamoja na Bunge la Dubai tuite Abudhabi ambapo ndiyo Makao Makuu ya *UAE* (Iran, Oman, Morocco na Mabunge mengine). Tutaweka karatasi pale katika Ofisi ya Katibu wa Bunge ili baadhi ya Wabunge ambao wangependa kuwa katika vyama vyaa urafiki na baadhi ya Mabunge, usijjandikishe Mabunge mengi, ni vizuri *at least* tukachagua Bunge moja na mwininge Bunge lingine ili baadaye tuone ni namna gani ya ku-link Mabunge haya kwa maana ya

kujifunza, wao kuja na sisi baadhi yetu kwenda katika Mabunge hayo kadri hali itakavyokuwa ikeruhusu.

La pili ambalo ni muhimu pia ni kwamba siku ya kesho itakuwa ni siku ya kipekee kwa Bunge baada ya tu ya kipindi cha maswali saa 4.30 asubuhi itabidi lazima maswali yaishe saa 4.30 asubuhi, maswali yakishaisha tutatoka hapa nje, patakuwa tameandalivawizuri na saa 5.00 asubuhi tutaanza kupokea taarifa za zile Kamati mbili ambazo niliziunda katika Bunge liliopita, Kamati inayojihusisha na masuala ya Almasi inayoongozwa na Mwenyekiti Mussa Azzan Zungu na Kamati iliyojishughulisha na masuala ya Tanzanite ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dotto Biteko. Kamati hizi ni za Bunge zitakuwa na taarifa ambazo ni muhimu na Mheshimiwa Waziri Mkuu tumemuomba awepo na amekubali, watawasilisha taarifa zile na mimi nikishazipokea pale pale nitamkabidhi Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote, Mawaziri, Naibu Waziri tushiriki katika shughuli hiyo na Taifa zima litakuwa likifuatilia kwa sababu itakuwa *televised live*. (*Makofii*)

Baada ya hapo nimesikia kuna mwongozo mmoja, Katibu niandikie majina.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE.DKT. SULEIMAN ALLY. YUSSUF: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Suleiman.

MHE.DKT. SULEIMAN ALLY. YUSSUF: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, nimeuliza maswali mawili ya nyongeza katika swali langu la msingi lakini bahati mbaya yote mawili hayakujibiwa. Bahati mbaya zaidi ni kwamba kasimama Waziri wa Mambo ya Ndani ambaye hata sheria

hazisomi kwa sababu nimempa kifungu cha *Tanzania Law Report* ya 1998...

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Suleiman unajua yaani sijui nisemeje, nachosisitiza hata kama unamhemuko kuhusu jambo fulani lakini jaribu kutulia. Ukitisema kwamba Waziri hata sheria hazisomi na nini inakuwa siyo kweli kwa ujumla wake yaani unaharibu hoja baada tu ya kuamua kupelekwa na jazba kidogo kwa hiyo tulia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. Ni kwamba nilisoma hapa *page* ya 48 ya *Tanzania Law Report* ya mwaka 1998 katika kesi ya Maalim Seif akishindana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kifungu kile kinasema wazi katika hukumu ya Mahakama ya Rufaa kwamba iwapo mtu atafanya kosa Zanzibar, hata kama kosa hilo linahusu Sheria ya Muungano basi kwanza atashitakiwa katika Mahakama ya Zanzibar, tena atashitakiwa Zanzibar na Mahakama ya Zanzibar. Kwa hiyo, jawabu alilolitoa si sahihi na halikubaliki.

Mheshimiwa Spika, lakini pia limeulizwa swali katika swali langu hilo hilo katika masuala ya *cybercrime*. Rafiki yangu Profesa Mbarawa kasema kwamba inawezekana hukumu hiyo pia kwenda Zanzibar. Tunavyojua ni kwamba Sheria yoyote ambayo inapitishwa hapa Bungeni haiwezi ikafanya kazi Zanzibar katika masuala ambayo si ya Muungano mpaka kwanza iridhiwe na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Tunaauliza, ni lini sheria hii ilipitishwa?

SPIKA: Maswali haya ni ya ufuatilaji. Suala la kwanza ambalo ndilo lilitusimamisha ni jambo ambalo liko mahakamani (ni kesi ambayo iko mahakamani hivi sasa) na mnajua taratibu za mihimili hii zinavyofanya kazi. Hata kuliruhusu lile swali nilipata taabu sana, lakini illibidi nivumilie tu niliache kwa sababu ni jambo ambalo liko mahakamani hivi sasa. Kwa hiyo, tunapo *query* uhalali wa kesi ambayo iko Mahakamani sisi Bunge na kuanza kujibu nadhani si sawasawa sana na kwa kuwa tulifanya si sawasawa sitaendeleza hiyo si sawasawa, kwa hiyo inabakia hapo.

Kuhusu haya mengine hebu jaribu kuwasiliana tu na Mheshimiwa Mbarawa pale mtazungumza na mtalimaliza. Hili la maswali na majibu kama hatujaridhika kwa kweli ni vizuri tukafuatilia kwa sababu Waheshimiwa Mawaziri ni Wabunge wenzetu; tukaona kama tunaweza tukapata majibu zaidi *unless ni issue* ambayo ni *completely critical*. Mheshimiwa Jesca Kishoa nilikuona kwa Mwongozo pia, nakupa nafasi.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) kwa niaba ya wanawake wote nchini pamoja na wanawake Wabunge wa Viti Maalum humu ndani bila kujali itikadi zetu za vyama.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. *Inconsistency* kwenye *leadership* ni kitu kibaya sana. Mwezi wa tatu mwaka huu Bunge liliopita katika kipindi cha maswali na majibu Mheshimiwa Sophia Mwakagenda aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Mambo ya Ndani kuhusiana na mikutano ya hadhara, akagusia Wabunge wa Viti Maalum na Serikali ikatoa majibu kwamba Wabunge wanaoruhusiwa kufanya mikutano ya hadhara ni Wabunge wa Majimbo, lakini pia na Waheshimiwa baunge wa Viti Maalum kwenye mikoa yao, wa majimbo kwenye majimbo yao na wale wa Viti Maalum kwenye Mikoa yao.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kauli hii kutoka Serikalini hivyo ndivyo ilivyokuwa. Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum waliendelea na mikutano, Wabunge wa majimbo waliendelea mikutano, lakini Wabunge wa Viti Maalum kwenye baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo limetokea jana, baada ya Mheshimiwa Waziri husika kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani kusema kwamba Wabunge wa Viti Maalum wanapaswa kufanya mikutano kwenye mikutano mikuu kwenye vyama vyao; moja, ni *inconsistency* ukilinganisha kwamba mwezi wa tatu alisema tofauti na alivyosema jana.

Mbili, ni kinyume na Katiba, *unconstitutional* kabisa; kwa sababu kwenye Katiba Wabunge wa Majimbo na Wabunge wa Viti Maalum wana haki sawa ndiyo maana tunalipwa mishahara inayofanana, lakini tatu ni ubaguzi wa waziwazi kwa wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo wako, kama leo utatutangazia rasmi humu ndani...

SPIKA: Nikurudishe kidogo Mheshimiwa Jesca ili twende vizuri, kidogo tu ili twende vizuri. Naomba ukae dakika moja tu ili twende vizuri kwa sababu jambo hili ni muhimu.

Tulikuwepo wote jana, alichosema Mheshimiwa Waziri kama nilimsikia vizuri lakini ye ye upo atanyoosha, ni kwamba mnaruhusiwa kuzungumza na wapiga kura wenu kule ambako ninyi ndio Wabunge wake. Mbunge wa Jimbo anajulikana wapiga kura wake ni watu gani. hivi Mbunge wa Viti Maalum unaenda kwenye mukutano wa hadhara, wale ndiyo wapiga kura wako? Wale walikuchagua lini? (*Makofi*)

Kwa hiyo, tuliweke vizuri, hayo mambo mengine wakati mwингine ni vizuri hata ukifanya labda nje kidogo ili tupate mjadala mpana. Endapo *concept* ni hiyo, sijui kama nilimuelewa vizuri Waziri au tumpe afafanue kwanza ili mwongozo wako uwemzuri?

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie.

SPIKA: Umalizie kwanza? Nakuruhusu, ahsante.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kauli ambayo aliitoa Mheshimiwa Waziri na ambayo hata wewe umekwenda kuisitiza basi ninakuomba mwongozo wako kwamba kuanzia sasa Wabunge wa Viti Maalum tutoe bendera zetu kwenye gari za Kibunge na tuweke bendera za vyama vyetu. Lakini pia tusiitwe Wabunge

wa Mikoa, tuitwe Wabunge wa mikutano mikuu ya vyama vyetu kwenye maeneo tunayotoka. (*Makofi*)

SPIKA: Kwani Jesca aliyesema ninyi ni Wabunge wa Mikoa ni nani? (*Kicheko*)

Yaani Katibu wa Bunge hapa ana nakala yoyote inayosema Mbunge fulani ametoka mkoa fulani? Hawa leo nimewaapisha hawa unaweza ukaniambia wanatoka mkoa gani? kuna hicho kitu? Hii habari ya Mikoa ni ya kwenu wenyewe hiyo, ni namna ya kupatikana kwenu lakini hakuna hicho kitu katika taratibu zetu sisi za Kibunge hapa. Wewe ni Mbunge wa Viti Maalum. Hii habari ya mikoa ni nyingine hiyo. Na nadhani mjadala huu tuuveke vizuri,

Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum kaeni kwa pamoja, nimwombe Mheshimiwa Waziri, siku hiyo hata mimi au hata Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaweza tukahudhuria kikao chenu, tukakutana pale Msekwa tukazungumza kwa undani tukaona hasa *issue* ni nini kwa undani wake maana mnawenza mkakariri tu.

Kuna watu hapa, nitoe mfano, kwa sababu yeye hatakasirika, Naibu Spika, wangu, yeye ni Mbunge wa mkoa gani? lakini si Mbunge? Kwa hiyo hapa tuna makundi, mkumbuke namna Bunge linavyokwenda kwa hiyo lazima tuangalie vizuri kidogo. Vinginevyo itakuwa shida kidogo.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

SPIKA: Kelele haisaidii, nadhani nimetao pendekezo zuri kwamba kutaneni, tukutane tulizungumze kwa mapana nadhani ni wazo zuri ili tuweze kulitatua likae vizuri, *otherwise* italeta taabu tu maana mimi kwenye rekodi zangu sina Mbunge wa mkoa wowote wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi kwa dakika mbili naomba nikupe nafasi kidogo kwa ufanuzi unaotaka kutoa.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Mheshimiwa Spika, sheria hii kweli tulipitisha mwaka 2015 na kawaida baada ya kuitisha Sheria hii inatakiwa ipelekwe Zanzibar, huko kwenye Baraza la Wawakilishi Zanzibar kikawaida haijadiliwi isipokuwa inawekwa mezani.

Mheshimiwa Spika, naomba tu nifuatilie kwa makini lakini ninavyoelewa mpaka sasa hivi sheria hiyo imeshapelekwa Baraza la Wawakilishi na ikishapelekwa Baraza la Wawakilishi, kinachofuata Sheria hii inaweza kutumika pande zote za Muungano.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, naomba nishukuru kwa ushirikiano wenu kwa kazi za leo asubuhi, baada ya hapa mnaenda katika katika Kamati zenu mbalimbali na kama tulivyo sema jana mambo yenu ya kuhusiana na kazi za ziada za Kamati yako sawasawa, yako vizuri, kwa hiyo, chapeni kazi.

Naahirisha shughuli za Bunge...

Ah! Kuna Miswada ya kusomwa kwa mara ya kwanza. Samahani sana, Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria
Mbalimbali Na.3 wa Mwaka 2017 [*The Written Laws
(Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2017*]**

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

**Muswada wa Sheria ya Reli wa Mwaka 2017
[*The Railways Bill, 2017*]**

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana Katibu. Sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 5.22 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 6 Septemba, 2017, Saa Tatu Asubuhi)